



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA RELI TANZANIA



Simu: 2133990
Telegramu: Railways
Nukushi: 2133428

Ofisi ya Uhusiano
S.L.P 70364
Dar es Salaam

TAARIFA KWA UMMA

**YAH: KUSITISHWA KWA HUDUMA ZA USAFIRI WA TRENI KUTOKA DAR ES
SALAAM KUELEKEA MIKOA YA BARA**

Dar es Salaam, Tarehe 28 Machi 2023

Shirika la Reli Tanzania (TRC) linautaarifu umma kusitishwa kwa huduma ya usafiri wa treni ya abiria inayotoka Dar es Salaam kuelekea mikoa ya bara (Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Tabora, Mwanza, Mpanda na Kigoma) kuanzia tarehe 28.03.2023.

TRC imesitisha utoaji wa huduma kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha sehemu mbalimbali nchini na kupelekea daraja kusombwa na maji kati ya stesheni ya Godegode na Gulwe, wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma.

Huduma ya treni inatarajia kurejea siku ya Alhamisi tarehe 30.03.2023. Shirika linaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza nakuendelea na jitihada za kuhakikisha huduma zinarejea haraka.

Jamila Mbarouk

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano